

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

### **TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA, KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA- DISEMBA ,2018)**

**Mhe, Mwenyekiti ,**

Kamati hii inaundwa na jumla ya Idara tano ,ambazo ni Afya,Maji, Elimu Msingi, Elimu Sekondari, na Maendeleo yya Jamii na Vijana. Kamati hii ilifanya kikao chake cha Kawaida cha Robo ya Pili mnamo tarehe 25.01.2018.

**Mhe, Mwenyekiti ,**

Kamati ilijadiliana taarifa za utekelezaji wa kila idara inayouunda kamati hii. Baada ya majadiliano hayo, kamati imeshauri na kuazimia yafuatayo;

- Kamati imeipongeza idara ya elimu msingi kwa kubaini jumla ya wanafunzi wanye mahitaji maalumu 255 ambao wanahitaji kupata elimu sawa kama wanafunzi wengine wasio na mahitaji maalum.
- Kamati ilipokea taarifa kutoka idara ya elimu Sekondari na kuitaka idara itoe nakala ya idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza na kuweza kufanya uhamasishaji wa karibu na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaendelea na masomo.
- Kamati iliagiza Idara ya Maji ikatoe elimu na kukamilisha kazi zinazofanywa kupitia Miradi ya Maji yenyeye vyombo huru vya

Watumia maji (COWSO) ili kuondoa muingiliano wa majukumu kati ya COWSO na wananchi.

**Mhe, Mwenyekiti ,**

Kamati pia imepokea taarifa kutoka Idara ya elimu msingi kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 kuna jumla ya walimu wa ajira mpya 31 waliopangwa na serikali kufundisha shule za msingi katika Halmashauri ya Mpwapwa, ambapo hadi sasa walioripoti ni 30 tangu tarehe 27,Disemba,2017 hadi terehe 7.Januari, 2018 ambapo ilikuwa mwishi wa kuripoti. Idara iendelee kufuatilia mwalimu mmoja ambaye hajarioti.

**Mhe, Mwenyekiti ,**

Naomba Baraza lako tukufu liweze kuridhia mapendekezo na maazimio haya yaliyoafikiwa.

.....  
**Mhe, JOCTAN CHELIGA**  
**MWENYEKITI KAMATI**  
**KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII**